

### 3- مَدُّ الْعَوَاضِ Maddul-'Iwadh

Ni madd inayotokea wakati wa kusimama msomaji katika neno lenye fat-hataan (tanwiyn fat-hah). Hukmu yake ni huvutwa kwa harakah mbili.

Mfano:

﴿ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً ..... ﴾<sup>1</sup>

Wakati wa kusimama kwenye neno فِرَاشًا ; بِنَاءً na مَاءً hubadilishwa tanwiyn ya fat-hataan na kuwa alif. Ama Inapounganishwa neno hutamkwa kutegemea na hukmu inayofuatia.

Linapounganishwa hutamkwa kwa tanwiyn	Lnaposimamiwa hubadilika tanwiyn ya fat-hataan na kuwa alif	Neno
sa'iyran	سَعِيرًا sa'iyra <b>a</b>	سَعِيرًا
Rahiyman	رَحِيمًا Rahiyma <b>a</b>	رَحِيمًا
Hudan	هُدَا Huda <b>a</b>	هُدَى
musamman	مُسَمًّا musamma <b>a</b>	مُسَمًّى
nisaaaaan	نِسَاءً nisaaaa <b>a</b>	نِسَاءً
maaaaaa	مَاءً maaaaa <b>a</b>	مَاءً
afwaajan	أَفْوَاجًا afwaaja <b>a</b>	أَفْوَاجًا

<sup>1</sup>Al-Baqarah (2: 22)

*Istithnaa* (Maneno yenye kwenda nje ya hukmu hii):

Kusimama kwenye ة (taa marbuwtwah ya kike iliyofungwa) kunapelekea kutokuwepo hukmu hii ya مَدُّ الْعَوْصِ (maddul-'iwadhw) kwani wakati huo huondoka tanwiyn na kusimamiwa kwa هَا (haa) saakinah<sup>2</sup>

Mfano:

مَغْفِرَةٌ      فَرِيضَةٌ      زَكَاةٌ

---

<sup>2</sup> Rejea mlango wa 'Kusimama kwenye mwisho wa neno'